

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA TANO

11 NOVEMBA, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA TANO – TAREHE 11 NOVEMBA, 2019

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**56. MHESHIMIWA MARY PIUS CHATANDA
(KOROGWE MJINI):**

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imefanya kazi kubwa sana ya ukarabati wa Shule ya Sekondari Korogwe lakini haikuunganisha nyumba za Walimu zilizopo Shuleni hapo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati nyumba hizo.

**57. MHESHIMIWA ZACHARIA PAUL ISSAAY
(MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sera ya Afya ni kuwa na Kituo cha Afya kwa kila Kata na Zahanati kwa

kila Kijiji; Tarafa ya Nambis katika Jimbo la Mbulu Mjini haina Kituo cha Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya kwenye Kata za Kainem, Murray, Nambis na Nahasey.

58. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kuna upungufu mkubwa wa Walimu katika Shule za Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu wa kutosha katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba.

59. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

(a) Je, ni nini sifa au vigezo vya kupata Halmashauri;

(b) Je, inachukua miaka mingapi kuendelea kuitwa Halmashauri ya Mji Mdogo hadi kuwa Halmashauri kamili.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

60. MHESHIMIWA DKT. RAPHAEL MASUNGA CHEGENI (BUSEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni nini maana ya dhana ya Uchumi kukua ukioanisha na maisha ya Wananchi.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

61. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Serikali imeanza Kampeni ya kusajili Watoto chini ya miaka mitano ili kupata vyeti vya kuzaliwa lakini bado Watanzania wenye umri zaidi ya miaka mitano na kuendelea hawana vyeti vya kuzaliwa:-

Je, Serikali imejipangaje kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa Watanzania wenye umri zaidi ya miaka mitano na kuendelea.

WIZARA YA KILIMO:

62. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-


Je, ni lini Serikali italetwa Muswada wa kudurusu Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2004.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

63. MHESHIMIWA GODFREY WILLIAM MGIMWA (KALENGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Kalenga kuelekea Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ni ya muhimu sana kwa uchumi wa Jimbo la Kalenga, Iringa na Tanzania kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya kuitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami.



WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

64. MHESHIMIWA MBAROUK SALIM ALI (WETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Pemba ni Kisiwa kinachozalisha viungo (*spices*) kwa wingi na Wajasiriamali huzalisha bidhaa zinazotokana na viungo hivyo:-

Je, ni lini Wakulima na Wajasiriamali wa Pemba wataunganishwa na soko la Afrika Mashariki ili waweze kufaidika na soko hilo.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

65. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi ni muhimu kwa mustakabali wa Afya za Wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa ugawaji wa fedha za mkupuo ili kuhakikisha ujenzi huo unakamilika.

66. MHESHIMIWA DKT. JASMINE TISEKWA BUNGA (VITI MAALUM)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Baadhi ya Watoto wakubwa wenye uwezo wameamua kuwatelekeza Wazazi wao pasipo kuwapa matunzo wanayostahili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawajibisha Watoto waliotelekeza Wazazi wao na kuhakikisha wanatoa matunzo stahili.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

67. MHESHIMIWA DEVOTA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Matukio ya watu kupoteza maisha kutokana na ajali za moto yamezidi kuongezeka nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiwezesha Kikosi cha Zimamoto ili kufanya kazi ipasavyo kwenye Miji na nje ya Miji.

68. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mfumo gani wa kupandisha madaraja Askari wenye vyeo vya chini.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

69. MHESHIMIWA JOYCE BITTA SOKOMBI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Kutokana na gharama za pango kuwa kubwa gharama za uendeshaji kwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere kilichopo Mkoani Mara zimeongezeka:-

Je, ni lini Serikali itakijengea Chuo hicho majengo yake na kuanza kuyatumia rasmi.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

70. MHESHIMIWA STANLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Serikali imeruhusu urasimishaji wa makazi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Jiji la Mwanza isipokuwa maeneo ya Kata za Isamilo, Mbugani, Mabatini na Igogo:-

Je, ni lini Serikali itawamilikisha Wananchi hawa maeneo yao kwa kuwa wameishi katika maeneo haya kwa muda mrefu.

III. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
11 NOVEMBA, 2019**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**